# KATIBA YA
# CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)

**TOLEO LA SITA LA MWAKA 2014**

Anwani ya Chama:

Chama cha Walimu Tanzania (CWT),
Mtaa wa Bwawani,
Kiwanja Na.42,
Manispaa ya Kinondoni,
S. L. P. 61110,
**DAR-ES-SALAAM.**

Simu: +255 22 276 2007
Nukushi: +255 22 276 1349

Barua pepe: info@ttu.or.tz

Tovuti: www.ttu.or.tz

# YALIYOMO


## SEHEMU YA KWANZA

**UTANGULIZI**

1. Jina
2. Anuani
3. Kauli Mbiu
4. Madhumuni
5. Fasiri

## SEHEMU YA PILI
## UANACHAMA NA MAADILI YA UALIMU

6. Wanachama
7. Haki na Wajibu wa Mwanachama
   - 7.1. Haki za Mwanachama Kamili
   - 7.2. Wajibu wa Mwanachama Kamili
   - 7.3. Haki za Mwanachama Shiriki
   - 7.4. Wajibu wa Mwanachama Shiriki
   - 7.5. Wajibu wa Mwanachama Maalum
8. Kujiandikisha kuwa Mwanachama kamili
9. Ukomo wa Uanachama
10. Maadili ya Ualimu

## SEHEMU YA TATU
## VIKAO NA MUUNDO WA UONGOZI

**11. Vikao vya Tawi Sehemu ya Kazi**
- 11.1 Mkutano Mkuu wa Tawi Sehemu ya Kazi
- 11.2 Taratibu za vikao katika Tawi Sehemu ya kazi
- 11.3 Kazi za Mkutano Mkuu wa Tawi Sehemu ya Kazi
- 11.4 Wajibu wa Katibu wa Tawi

**12. Kazi na Madaraka ya Mwenyekiti Sehemu ya Kazi**

**13. Vikao vya Ngazi ya Wilaya**
- 13.1 Mkutano Mkuu wa Wilaya
- 13.2 Kamati ya Utendaji ya Wilaya
- 13.3 Kamati ya Uendeshaji ya Wilaya

**14. Taratibu za Vikao vya Wilaya**

14.1 Mkutano Mkuu wa Wilaya
14.2 Kamati ya Utendaji ya Wilaya
14.3 Kamati ya Uendeshaji ya Wilaya

**15. Wajibu wa Vikao vya Wilaya**
15.1 Mkutano Mkuu wa Wilaya
15.2 Kamati ya Utendaji ya Wilaya
15.3 Kamati ya Uendeshaji ya Wilaya

**16. Kazi na Madaraka ya Viongozi wa Wilaya**
16.1 Mwenyekiti
16.2 Katibu
16.3 Mweka Hazina

**17. Wajumbe wa Ngazi ya Mkoa**
17.1 Mkutano Mkuu wa Mkoa
17.2 Baraza la Mkoa
17.3 Kamati ya Uendeshaji ya Mkoa

**18. Taratibu za Vikao vya Mkoa**
18.1 Mkutano Mkuu wa Mkoa
18.2 Baraza la Mkoa
18.3 Kamati ya Uendeshaji ya Mkoa

**19. Wajibu wa Vikao vya Mkoa**
19.1 Mkutano Mkuu wa Mkoa
19.2 Baraza la Mkoa
19.3 Kamati ya Uendeshaji ya Mkoa

**20. Kazi na Madaraka ya Viongozi wa Mkoa**
20.1 Mwenyekiti
20.2 Katibu
20.3 Mweka Hazina

**21. Wajumbe wa Ngazi ya Taifa**
21.1 Mkutano Mkuu wa Taifa
21.2 Baraza la Taifa
21.3 Kamati ya Utendaji ya Taifa

**22. Taratibu za Vikao vya Taifa**
22.1 Mkutano Mkuu wa Taifa
22.2 Baraza la Taifa

22.3 Kamati ya Utendaji ya Taifa

**23. Wajibu wa Vikao vya Taifa**
23.1 Mkutano Mkuu wa Taifa
23.2 Baraza la Taifa
23.3 Kamati ya Utendaji ya Taifa

**24. Kazi na Madaraka ya Viongozi wa Taifa**
24.1 Rais
24.2 Makamu wa Rais
24.3 Katibu Mkuu
24.4 Naibu Katibu Mkuu
24.5 Mweka Hazina

25. Wadhamini wa Chama
26. Kitengo cha Walimu Wanawake
27. Kitengo cha Walimu wenye Ulemavu
28. Taratibu za kuitisha Vikao
29. Uchaguzi na muda wa Uongozi
30. Watumishi wa Chama

## SEHEMU YA NNE
## FEDHA NA MALI ZA CHAMA

31. Mapato ya Chama
32. Matumizi ya fedha za Chama
33. Taratibu za utunzaji wa fedha za Chama
34. Bajeti ya mwaka ya Chama
35. Mali za Chama

## SEHEMU YA TANO
## MENGINEYO:

36. Kupiga kura
37. Utatuzi wa Migogoro
38. Tafsiri ya Katiba
39. Mabadiliko ya Katiba
40. Kanuni za Chama
41. Muda wa kukaimu
42. Kufukuzwa Uanachama
43. Kujaza nafasi zilizo wazi za uongozi
44. Tawi la Wafanyakazi.

45. Kufuta Chama cha Walimu Tanzania (CWT)
46. Mgomo
47. Kuungana na au kuunda Shirikisho

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

**KWA KUWA** sisi Walimu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunalo jukumu kubwa la kuelimisha Umma na kutayarisha viongozi wazuri wa leo na kesho wa nchi hii;

**KWA KUWA** kazi ya Ualimu inahitaji elimu, ujuzi, ufahamu, uadilifu, uvumilivu na upendo;

**KWA KUWA** Mwalimu kama raia mwingine yeyote nchini ana haki ya kupata huduma bora za kijamii, kiuchumi na kimaslahi kama vile afya, chakula, malazi, usafiri na huduma nyingine za kijamii;

**KWA HIYO BASI,** sisi Walimu wote kwa pamoja tunaazimia kuungana na kuunda Chama chetu kitakachohakikisha kuwa Walimu wote tunatekeleza wajibu wetu na kupata haki zote tunazostahili kutoka kwa Waajiri wetu.

### 1. JINA

Jina la Chama litakuwa:
CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)/TANZANIA TEACHERS' UNION (TTU)

### 2. ANUANI

KATIBU MKUU,
CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT),
MTAA WA BWAWANI,
KIWANJA NA. 42,
MANISPAA YA KINONDONI,
S.L.P. 61110,
DAR- ES -SALAAM.

### 3. KAULI MBIU

"Wajibu na Haki"

## 4. MADHUMUNI

(a) Kuendeleza na kulinda hadhi ya kazi ya Ualimu pamoja na kusimamia viwango vya juu vya maadili, ufahamu, maarifa na ujuzi.

(b) Kusimamia, kuendeleza na kulinda maslahi ya Walimu na Watendaji, katika Taasisi za Elimu na kuhakikisha kuwa kuna vivutio vya kutosha na mazingira mazuri ya kuwafanya waipende na kuizingatia kazi yao.

(c) Kuhimiza elimu na ujuzi wa Watendaji wanaohudumia Shule, Vyuo na sehemu zote zinazoshughulikia elimu.

(d) Kuwa kitovu cha maandiko ya kuwaendeleza Walimu, Wanachama na Wananchi katika elimu na mafunzo ya kazi ya Ualimu.

(e) Kuwahimiza Walimu kufanya kazi yao vizuri na kuwasisitiza waoneshe mfano bora wa kazi, uadilifu, tabia na mwenendo.

(f) Kuwakutanisha Walimu mara kwa mara ili waweze kujadili maendeleo na matatizo katika taaluma zao na kutafuta mbinu za kuyatatua, kufahamiana na kubadilishana mawazo ili kujenga utamaduni wa kujiendeleza.

(g) Kuhimiza na kuhakikisha kuwa Walimu na Watendaji wanapata huduma zote wanazostahili kiuchumi, kiafya na kijamii.

(h) Kujadili na kushauriana na Waajiri juu ya haki, maslahi na hali nyingine zinazohusiana na mazingira ya ajira ya Ualimu.

(i) Kuishauri serikali juu ya mambo mbalimbali yanayohusu maendeleo ya elimu nchini.

(j) Kuhakikisha kuwa waajiri wanaohusika wanatambua uwepo wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) na kuwaelimisha Walimu kuwa wana uhuru wa kujiunga na Chama hicho na uhuru wa kufanya mgomo pale inapobidi.

(k) Kusuluhisha migogoro na kutatua malalamiko mahali pa kazi kati ya Waajiri na Walimu au miongoni mwa Walimu wenyewe.

(l) Kutunga na kusimamia Sera itakayolinda hadhi ya Walimu wanawake kwa kutambua hali na maumbile yao na kuhakikisha kuwa afya zao zinalindwa bila ubaguzi wa ajira, likizo ya uzazi na huduma nyingine anazostahili Mwalimu yeyote.

(m) Kutunga na kusimamia Sera itakayolinda hadhi ya Walimu wenye ulemavu kwa kutambua hali, maumbile na mazingira yao ya kazi .

(n) Kuhakikisha kuwa katika sehemu zote za kazi Walimu hawapati bughudha ya kijinsi na kuweka utaratibu utakaodhibiti wale watakaokiuka.

(o) Kuhakikisha kuwa waajiri na Walimu wanazingatia na kutekeleza sheria na kanuni za nchi zinazohusu kazi, pamoja na mikataba iliyopo kati ya waajiri hao na Walimu au Chama cha Walimu ili mradi sheria hizo zinazingatia HAKI.

(p) Kuwaelimisha wanachama juu ya masuala yote yanayohusiana na ajira zao ikiwa ni pamoja na kuwapa ushauri wa kisheria unapohitajika.

(q) Kuhakikisha kwamba hakuna ubaguzi wa rangi, kabila, dini, jinsi, ulemavu au hali miongoni mwa wanachama.

(r) Kuwa na uhuru wa kushirikiana na kushauriana na vyama vingine vya wafanyakazi nchini na nje ya nchi.

(s) Kuwekeza katika vitega uchumi vitakavyoboresha ustawi wa wanachama ingawa si Chama cha Kibiashara.

(t) Kutengeneza na kutetea Sera itakayolinda hadhi ya Walimu wenye ulemavu na kuhakikisha kuwa afya zao na vikwazo vinavyoathiri utendaji wao vinaondolewa na kupata huduma nyingine wanazostahili Walimu wenye ulemavu.

## 5. FASIRI

Mahali popote ambapo maneno yanayotamkwa hapa chini yametumika katika Katiba hii, yana maana au ufafanuzi au fasiri iliyotolewa juu yake na katiba hii.

- **Akidi –**Ni idadi ya wajumbe wanaotakiwa ili kikao kianze.
- **Baraza la Wadhamini -** Chombo cha wadhamini wa Chama chenye wajumbe watatu.
- **Bendera ya Chama -** Alama ya Chama yenye rangi ya njano, nyeupe na nembo ya Chama. Kanuni za Chama zitafafanua maana ya alama zilizotumika kwenye Bendera ya Chama.
- **Chama** -Ni Chama cha Walimu Tanzania(CWT) au 'Tanzania Teachers' Union'(TTU)
- **Kanuni -** Taratibu zinazoitafsiri Katiba na kutoa mwongozo wa utekelezaji wake.
- **Katiba -** Kanuni za msingi ambazo kwazo Chama kinaendesha shughuli zake.
- **Katibu -** Mtendaji Mkuu wa shughuli za Chama katika ngazi husika.
- **Katibu Mkuu** - Mtendaji Mkuu wa Chama au Afisa mwingine ambaye ameidhinishwa na Katibu Mkuu kutenda shughuli kwa niaba yake.
- **Kiongozi** - Mwanachama yeyote aliyechaguliwa na Chama au kuajiriwa na Chama kushika nafasi yoyote ya uongozi katika Chama.
- **Mfanyakazi -** Mtu aliyeingia katika makubaliano au mkataba wa maandishi na mwajiri yeyote yule kwa kutenda kazi kwa kupewa fidia/malipo ya ajira au mshahara kwa kila juma, majuma au mwezi mwajiri huyo.

- **Mgogoro -** Kuwepo hali isiyokuwa ya maelewano kati ya mwajiri na mfanyakazi au wafanyakazi kuhusu ajira.

- **Mgomo -** Kitendo chochote kinachotendwa na Wafanyakazi ambacho kitasababisha uzorotaji kazi kutokana na kutoelewana kati ya mwajiri na wafanyakazi kuhusu hali na masharti ya kazi.

- **Mgomo wa kuketi –** Ni mgomo wa kuweka chini zana za kazi ambapo wafanyakazi huenda kazini lakini hawafanyi kazi yoyote bali huketi kitako.

- **Mgomo wa wafanyakazi** - Wafanyakazi kukataa kufanya kazi mpaka hapo madai yao ya yatakapokubaliwa na mwajiri.

- **Mkataba wa hiari -** Makubaliano yaliyofikiwa kati ya Chama cha wafanyakazi na Mwajiri au Chama cha waajiri kuhusu haki na mazingira bora ya kazi na maslahi.
- **Mkoa -** Mkoa wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) ni kama itakavyoamuliwa mara kwa mara na Baraza la Taifa.

- **Mwajiri -** Mtu binafsi, Kampuni, Shirika, Serikali ambayo imeingia katika makubaliano/mkataba wa maandishi na mtu fulani kwa madhumuni ya kumtendea kazi kwa kutoa fidia au malipo ya ajira au mshahara.

- **Mwalimu -** Mfanyakazi yeyote mwenye taaluma na mafunzo ya ualimu, na wale wenye leseni za kufundishia.

- **Mwalimu kijana –** Ni mwanachama kamili mwenye umri kati ya miaka 18 hadi 35.

- **Mwanachama -** Mwalimu au Mtumishi wa Chama anayetoa ada kila mwezi na kusajiliwa, Mwalimu mstaafu, Mkurufunzi na mtu mashuhuri ambaye atakuwa ametoa mchango maalum

katika taaluma ya ualimu na kuthibitishwa na Chama.

- **Mweka Hazina -** Mtunza Hazina wa Chama katika ngazi husika.

- **Mwenyekiti** - Kiongozi Mkuu wa Chama katika ngazi husika.

- **Naibu Katibu Mkuu -** Mtendaji Mkuu Msaidizi wa Chama.

- **Rais -** Kiongozi Mkuu wa Chama.

- **Sera -** Dira ya Chama inayotoa mwelekeo na mwongozo wa shughuli zote za Chama.

- **Shule, Chuo au Taasisi** - Sehemu za kazi zenye wanachama wa Chama cha Walimu Tanzania na inajumuisha shule za Awali, Msingi, Sekondari, Vyuo vya Ualimu, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi na Ofisi za serikali zenye wanachama. Hii inahusisha Taasisi za serikali na zisizo za serikali.

- **Taasisi -** Ni sehemu au mamlaka yoyote inayoshughulikia masuala ya utoaji wa elimu.

- **Taifa –** Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

- **Tawi la Chama** – Kila Shule, Chuo au Taasisi itakuwa ni Tawi la Chama cha Walimu Tanzania

- **Ulemavu –** Ni kukosa au kushindwa kuwa na fursa ya kushiriki katika maisha ya kawaida ya kijamii sawa na watu wengine kwa sababu za kimaumbile, kiakili au sababu za kijamii.

- **Wadhamini -** Wanachama kamili waaminifu waliochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa na kupewa dhamana ya kuwa wamiliki wa mali na fedha za Chama kwa niaba ya Chama.

- **Wilaya -** Wilaya ya Chama ni kama itakavyoamuliwa na Baraza la Taifa.

## SEHEMU YA PILI

## UANACHAMA NA MAADILI YA UALIMU

### 6. MWANACHAMA

#### 6.1 Mwanachama Kamili

(a) Mwalimu mwenye sifa ya taaluma ya ualimu

(b) Mwalimu mwenye leseni ya kufundisha.
(c) Anayelipa Ada ya Uanachama kila mwezi

#### 6.2 Mwanachama Shiriki

(a) Mwalimu mwenye Taaluma ya Ualimu ambaye anaishi na kufanya kazi nje ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
(b) Mkurufunzi katika Chuo kinachotoa mafunzo ya ualimu.

(c) Mwalimu mstaafu.

(d) Mwalimu mwenye umri wa zaidi ya miaka sitini (60)

#### 6.3 Mwanachama wa Heshima

Uanachama wa Heshima utatolewa na Baraza la Taifa kwa mtu mashuhuri ambaye ametoa mchango maalum katika taaluma ya ualimu.

#### 6.4 Mwanachama Maalum

Mwanachama Maalum atakuwa ni mwajiriwa wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT).

### 7. HAKI NA WAJIBU WA MWANACHAMA

7.1 Haki za Mwanachama kamili:

(a) Kuchagua na kuchaguliwa kushika nafasi ya uongozi wa Chama.
Mwanachama atashika nafasi moja tu ya uongozi/uwakilishi ndani ya Chama katika kipindi kimoja isipokuwa katika uwakilishi nje ya Chama.

(b) Kujitetea na kutoa maelezo mbele ya kikao cha Chama au chombo kinachohusika katika mashitaka yoyote yaliyotolewa dhidi yake.

(c) Kukata rufaa ya kwenda katika kikao cha juu cha Chama, endapo mwanachama hakuridhika na uamuzi uliotolewa dhidi yake. Kwa matatizo ya kichama isipokuwa kwa ngazi ya mkoa rufaa itaishia katika Baraza la Mkoa. Kwa matatizo ya Kiongozi isipokuwa viongozi wanaochaguliwa na Mkutano Mkuu wa Taifa rufaa ya mwisho itaishia katika Baraza la Taifa.

(d) Kutetewa na Chama kuhusu haki na maslahi yake yanayohusu kazi yake kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa.

(e) ushiriki na kufaidi matunda yote yatokanayo na shughuli za kitaaluma, ushirika na ustawi wa jamii zinazoendeshwa na Chama kwa mujibu wa Kanuni au Sheria na Taratibu zilizowekwa.

(f) Kuelimishwa kuhusu haki zake.

## 7.2 Wajibu wa Mwanachama Kamili

(a) Kulipa ada ambayo ni asilimia mbili (2%) ya mishahara wa Mwanachama kabla ya makato au kwa kiwango kitakachoamuliwa na Baraza la Taifa na itakatwa kupitia 'check off system' au kama itakavyoamuliwa na Baraza la Taifa.

(b) Kuhudhuria vikao vya Chama vinavyohusika.

(c) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za Chama.

(d) Kutekeleza maamuzi ya Chama.

(e) Kujiendeleza kielimu na kitaaluma kwa uwezo wake wote.

(f) Kujua haki zake.

(g) Kukilinda, kukitangaza na kukitetea Chama wakati wote na kwa nguvu zote.

### 7.3 Haki za Mwanachama shiriki

(a) Kutetewa na Chama kuhusu maslahi yake yanayohusu kazi yake kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa.

(b) Kujitetea na kutoa maelezo mbele ya kikao cha Chama au chombo kinachohusika katika mashitaka yaliyotolewa dhidi yake.

(c) Kukata rufaa ya kwenda katika kikao cha juu cha Chama, endapo mwanachama hakuridhika na uamuzi uliotolewa dhidi yake. Kwa matatizo ya kichama rufaa itaishia katika Baraza la Taifa.

(d) Kushiriki na kufaidi matunda yote yatokanayo na shughuli za kitaaluma, ushirika na ustawi wa jamii zinazoendeshwa na Chama kwa mujibu wa sheria au kanuni na taratibu zilizowekwa.

### 7.4 Wajibu wa Mwanachama shiriki

(a) Kushauri na kutoa mawazo ya kukiendeleza Chama.

(b) Kujielimisha na kukielewa Chama.

(c) Kuunga mkono juhudi zote za Chama.

(d) Kuendeleza maadili ya kazi ya Ualimu.

### 7.5 Haki za mwanachama maalum

(a) Kutetewa na Chama kuhusu maslahi yake yanayohusu kazi yake kwa mujibu wa Sheria na taratibu zilizowekwa.

(b) Kujitetea na kutoa maelezo mbele ya kikao cha Chama au Chombo kinachohusika.

(c) Kukata rufaa ya kwenda katika kikao cha juu cha Chama endapo hakuridhika na uamuzi uliotolewa dhidi yake.

(d) Kushiriki na kufaidi matunda yote yatokanayo na shughuli za Chama.

### 7.6 Wajibu wa Mwanachama Maalum

(a) Kulipa ada ambayo ni asilimia mbili (2%) ya mshahara wa mwanachama kabla ya makato au kiwango kitakachoamuliwa na Baraza la Taifa na itakatwa moja kwa moja kutoka kwenye mshahara (Check off system) au kama itakavyoamuliwa na Baraza la Taifa.

(b) Kuhudhuria vikao vya Chama vinavyohusika.

(c) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za Chama.

(d) Kutekeleza shughuli za Chama.

(e) Kujiendeleza kwa uwezo wake wote kielimu na kitaaluma.

(f) Kujua haki zake.

(g) Kulinda, kukitangaza na kukitetea Chama wakati wote na kwa nguvu zote.

## 8 KUANDIKISHWA UANACHAMA KAMILI

Mwanachama ataorodheshwa katika daftari kuu la Chama kwa jina lake kamili na **taarifa** nyingine zinazomhusu.

## 9 KUKOMA UANACHAMA

### 9.1 Mwanachama atakoma Uanachama kamili iwapo:

(a) Hakutoa ada yake kwa kipindi cha miezi 12 mfululizo bila sababu zinazohusiana na ajira yake.

(b) Hatakuwa mfanyakazi wa kuajiriwa kwa kuacha, kuachishwa kazi au kufukuzwa kazi na Chama kuridhika kuwa kufukuzwa kwake ni halali.

(c) Atajiuzulu.

(d) Atashindwa kutimiza maadili ya ualimu.

(e) Atafukuzwa Uanachama.

(f) Atafariki dunia.

(g) Atastaafu.

(h) Atatimiza umri wa miaka 60.

**9.2 Mwanachama akikoma uanachama hatarudishiwa ada zake.**

## 10 MAADILI YA UALIMU

Mwanachama ni lazima azingatie maadili ya kazi ya ualimu kama yalivyo katika sheria za nchi ili mradi zinazingatia HAKI.

## SEHEMU YA TATU

## VIKAO, MUUNDO NA UONGOZI WA CHAMA NGAZI YA TAWI

## 11 KIKAO VYA TAWI SEHEMU YA KAZI

### 11.1 Mkutano Mkuu wa Tawi

Mkutano Mkuu wa Tawi Sehemu ya Kazi wa wanachama utakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti wa Tawi Sehemu ya Kazi ambaye atachaguliwa na wanachama wote waliohudhuria kikao kwa ajili ya kuendesha kikao hicho tu.
(b) Mwakilishi wa sehemu ya kazi ambaye atakuwa ni Katibu

(c) Wanachama wote walio katika sehemu ya kazi

### 11.2 . Utaratibu wa vikao vya Tawi katika sehemu ya kazi

(a) Kutakuwa na vikao vitatu vya vya Mkutano Mkuu wa Tawi Sehemu ya Kazi kwa mwaka.

(b) Vikao vya dharura vinaweza kuitishwa umuhimu unapojitokeza.

(c) Kabla ya kikao kuanza katika Tawi Sehemu ya Kazi , wajumbe watamteua Mwenyekiti kutoka miongoni mwa wanachama waliohudhuria kuongoza kikao husika na muda wake wa uongozi utakoma baada ya kufungwa au kuahirishwa kwa kikao.

### 11.3 Kazi ya Mkutano Mkuu wa Tawi Sehemu ya Kazi

(a) Kujadili na kupitisha bajeti na mipango ya mwaka ya kazi za Chama Sehemu ya kazi
(b) Kupokea na kujadili taarifa za Chama kwa kipindi cha miezi minne.
(c) Kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Chama kwa kipindi cha miezi minne.

(d) Kupokea na kujadili taarifa mbalimbali zilizowasilishwa kutoka ngazi za juu za Chama.
(e) Kusimamia utekelezaji wa maamuzi ya Chama ya ngazi za juu.
(f) Kuchagua Mwakilishi wa Sehemu ya Kazi ambaye atakuwa ni Katibu wa Tawi Sehemu ya Kazi.
(g) Kujadili masuala mbalimbali yanayohusu Chama na wanachama.
(h) Kubuni njia mbalimbali za kuimarisha Chama na ustawi wa wanachama.
(i) Kumwondoa madarakani Mwakilishi wa Sehemu ya Kazi ambaye pia ni Katibu akipatikana na hatia baada ya kupewa fursa ya kusikilizwa.

## 11.4 Wajibu wa Katibu wa Tawi Sehemu ya Kazi

(a) Kiongozi Mkuu wa Chama katika Tawi.
(b) Kuwa kiungo kati ya ofisi ya Shule, Chuo au Taasisi na Wanachama juu ya haki zao za Chama kitaaluma na majukumu yao ya kiualimu.

(c) Kusimamia masuala ya usajili wa wanachama na kuhakikisha kuwa wanadumu katika Chama

(d) Kuwawakilisha wanachama katika migogoro ya kikazi na ya masuala ya kinidhamu pamoja na kusimamia utatuzi wa migogoro ya wanachama sehemu za kazi.

(e) Kukiwakilisha Chama katika uchunguzi wa utekelezaji wa Sheria za kazi unaoendeshwa na wakaguzi wa kazi.

(f) Kuwawakilisha wanachama katika masuala ya afya, usalama kazini na ustawi wa jamiii.

(g) Kupokea maagizo au taarifa kutoka ngazi ya wilaya, kusimamia utekelezaji wake na kutoa mwitiko kwa uongozi wa Wilaya

(h) Kuwajibika kwa ngazi zilizopo juu yake

(i) Kuhimiza na kuelimisha wanachama juu ya masuala ya Chama, wajibu na haki zao.

(j) Kuimarisha mawasiliano ya moja kwa moja kati ya Shule na ofisi ya Chama ya Wilaya.

(k) Kusimamia na kuhimiza demokrasia katika shule, Chuo au Taasisi.

(l) Kuhamasisha wanachama kikamilifu katika masuala ya Vyama vya Wafanyakazi na taaluma ili kuleta maisha na hali bora kwa wanachama.

(m) Kuandaa taarifa ya shughuli za Chama katika kipindi husika.
(n) Kuitisha vikao vya Chama vya Tawi
(o) Kusimamia shughuli zote za uendeshaji ikiwa ni pamoja na mapato na matumizi ya fedha za chama.
(p) Kutunza mali zote za Chama.
(q) Kuwa Katibu wa Vikao vya Mikutano ya Tawi.
(r) Kuweka kumbukumbu za shughuli za Chama katika Tawi.
(s) Kusajili wanachama
(t) Kuandaa na Kutunza kumbukumbu za wanachama
(u) Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya mapato na matumizi ya sehemu ya kazi.
(v) Kuwa msemaji na mtetezi Mkuu wa Chama katika Tawi.
(w) Kutoa msimamo na Sera za Chama kama itakavyoamuliwa na vikao vya Chama Kitaifa.
(x) Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya

**12. Kazi na Madaraka ya Mwenyekiti wa Tawi Sehemu ya Kazi**

(i) Kuwa Mwenyekiti wa kikao husika
(ii) Kuendesha kikao kwa kuzingatia Katiba na Kanuni zake.

## 13. VIKAO VYA WILAYA

### 13.1. Mkutano Mkuu wa Wilaya

Mkutano Mkuu wa Wilaya utakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Wilaya.

(b) Mwakilishi kutoka katika kila Shule, Chuo au Taasisi zenye wanachama zilizoko kwenye Wilaya husika.

(c) Wajumbe wa vikao vya juu vya Chama walioko kwenye Wilaya husika isipokuwa Rais, Makamu wa Rais, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Mweka Hazina wa Taifa

### 13.2. Kamati ya Utendaji ya Wilaya

Kamati ya Utendaji ya Wilaya itakuwa na wajumbe Wafuatao:-

(a) Wajumbe wa Kamati ya Uendeshaji ya Wilaya
(b) Mwenyekiti wa Kitengo cha Walimu wanawake Wilaya -1
(c) Wawakilishi wa walimu wa shule za msingi -4
(d) Wawakilishi wa walimu wa shule za sekondari -2
(e) Mwakilishi wa Vyuo vya Ualimu 1
(f) Mwakilishi wa Vyuo vya Maendeleo ya wananchi -1
(g) Mwakilishi wa Vyuo vya Maendeleo ya wananchi -1
(h) Mwakilishi wa Shule/Vyuo Binafsi - 1
(i) Mwakilishi kutoka Taasisi za Uongozi – 1
(j) Mwakilishi kutoka Shule za Awali – 1

### 13.3. Kamati ya Uendeshaji ya Wilaya

Kamati ya Uendeshaji ya Wilaya itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(i) Mwenyekiti wa Wilaya.
(ii) Katibu wa Wilaya
(iii) Mweka Hazina wa Wilaya.
(iv) Mwakilishi wa Walimu wenye ulemavu wa Wilaya. Mwakilishi wa Walimu wanawake wa Wilaya .
(v) Mwakilishi wa Walimu vijana wa Wilaya

## 14. TARATIBU ZA VIKAO KATIKA NGAZI YA WILAYA

### 14.1 . Mkutano Mkuu wa Wilaya

Mkutano Mkuu wa Wilaya utafanyika kila baada ya miaka miwili na nusu.

### 14.2 Kamati ya Utendaji ya Wilaya

(a) Kamati ya Utendaji ya Wilaya **itakutana** mara **mbili** kwa mwaka.

(b) Mikutano ya dharura inaweza kuitishwa iwapo wajumbe wasiopungua nusu (1/2) ya wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Wilaya wataomba kwa maandishi.

### 14.3 Kamati ya Uendeshaji ya Wilaya

(a) Kamati ya Uendeshaji ya Wilaya itakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu.

(b) Tarehe ya mkutano itapangwa na Katibu kwa kushauriana na Mwenyekiti.

## 15. WAJIBU WA VIKAO VYA WILAYA

### 15.1 Mkutano Mkuu wa Wilaya

Kazi za Mkutano Mkuu wa Wilaya zitakuwa kama ifuatavyo:

(a) Kupokea na kujadili taarifa ya kazi ya Chama kwa kipindi cha miaka mitano kama ilivyowasilishwa na Kamati ya Utendaji ya Wilaya.

(b) Kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya fedha kwa kipindi cha miaka mitano kama itakavyowasilishwa na Kamati ya Utendaji ya Wilaya.

(c) Kuchagua viongozi wafuatao ngazi ya Wilaya:-

(i) Mwenyekiti wa Wilaya

(ii) Mweka Hazina wa Wilaya

(iii) Mwakilishi wa Walimu Wanawake Wilaya

(iv) Mwakilishi wa Shule za Awali - 1

(v) Mwakilishi wa Shule za Msingi -4

(vi) Mwakilishi Shule za Sekondari -2

(vii) Mwakilishi Vyuo vya Ualimu - 1

(viii) Mwakilishi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi-1

(ix) Mwakilishi wa Uongozi na Taasisi nyingine za Elimu-1

(x) Mwakilishi wa Walimu wenye ulemavu Wilaya – 1

(xi) Mwakilishi wa Walimu vijana Wilaya – 1

(d) Kupokea, kujadili na kuthibitisha mipango ya miaka mitano ya Chama ngazi ya Wilaya.

(e) Kuwaondoa madarakani viongozi uliowachagua wakipatikana na hatia baada ya kuwapa fursa ya kusikilizwa.

**15.2 Kamati ya Utendaji ya Wilaya**

(a) Kupokea, kujadili na kuthibitisha taarifa ya kazi ya Chama kwa kipindi cha mwaka mmoja kama ilivyowasilishwa na Kamati ya Uendeshaji ya Wilaya.

(b) Kupokea, kujadili na kuthibitisha taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Chama kama ilivyowasilishwa na Kamati ya Uendeshaji ya Wilaya.

(c) Kuandaa agenda za Mkutano Mkuu wa Wilaya.

(d) Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa Wilaya.

(e) Kuandaa na kutekeleza Mpango Mkakati wa miaka miwili na nusu

(f) Kujaza nafasi zilizo wazi za uongozi wa Wilaya.

(g) Kuendeleza na kusimamia shughuli za Chama ikiwa ni pamoja na mapato na matumizi ya Chama.

(h) Kusimamia utekelezaji wa maazimio ya vikao vya juu vya Chama.

(i) Kudhibiti mapato na matumizi ya fedha za Chama na kutoa taarifa kwa Mkutano Mkuu wa Wilaya.

(j) Kubuni na kusimamia uendeshaji wa Miradi ya kiuchumi ya Chama katika Wilaya.

(k) Kushughulikia maendeleo ya walimu katika maslahi yao, elimu na mafunzo, uimarishaji wa Chama, afya kazini, usafi wa mazingira na mengineyo katika kuinua hadhi na taaluma ya Ualimu.

(l) Kumsimamisha uongozi Kiongozi wa kuchaguliwa atakayebainika kukiuka taratibu za Chama au kufanya ubadhirifu wa mali na fedha za Chama katika ngazi ya Wilaya na kumpeleka katika Mkutano Mkuu wa Wilaya kwa hatua zaidi.

**15.3 Kamati ya Uendeshaji ya Wilaya**

(a) Kuendesha na kusimamia shughuli za Chama Wilayani.

(b) Kusimamia utekelezaji wa maazimio ya vikao vya juu.

(c) Kudhibiti na kuandaa taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Chama na kutoa taarifa kwa Kamati ya Utendaji ya Wilaya.

(d) Kupitia Utekelezaji wa Mpango wa Kazi kila baada ya miezi mitatu.

(e) Kuratibu shughuli zote za Chama za Wilaya.

(f) Kudhibiti fedha na mali za Chama katika Wilaya.

## 16. KAZI NA MADARAKA YA VIONGOZI WA NGAZI YA WILAYA

### 16.1 Mwenyekiti

(a) Kiongozi Mkuu wa Chama katika Wilaya.

(b) Kuwa mwenyekiti wa vikao vyote vya Chama vya Wilaya.

(c) Kuwa msemaji na mtetezi mkuu wa Chama katika Wilaya.

(d) Kutoa msimamo na kutetea Sera za Chama kama itakavyoamuliwa na vikao vya Chama kitaifa.

(e) Kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya vikao vyote vya Chama.

### 16.2 Katibu

(a) Kuitisha vikao vya Chama vya Wilaya kwa kushauriana na Mwenyekiti.

(b) Kusimamia shughuli zote za uendeshaji ikiwa ni pamoja na mapato na matumizi ya fedha za Chama.

(c) Kutunza mali zote za Chama.

(d) Kuwa Katibu wa Vikao na Mikutano ya Wilaya.

(e) Kuweka kumbukumbu za shughuli za Chama katika Wilaya.

(f) Kufuatilia makato ya Ada za wanachama na Ada za Huduma kutoka kwa waajiri.

(g) Mtendaji Mkuu wa Chama katika Wilaya.

(h) Kuandaa taarifa ya shughuli za Chama katika kipindi husika.

(i) Kufuatilia marejesho ya Ada za wanachama kutoka kwa Katibu wa Mkoa.

### 16.3 Mweka Hazina

(a) Kuandaa na kutoa taarifa za fedha za Chama katika vikao vya Wilaya kwa kushirikiana na Katibu.

(b) Kubuni mbinu za kuongeza mapato ya Chama katika ngazi ya Wilaya.

(c) Kuweka kumbukumbu sahihi za mapato na matumizi ya Chama.

(d) Atakuwa ndiye Kaimu Katibu wa Wilaya.

## 17. WAJUMBE WA NGAZI YA MKOA

### 17.1 Mkutano Mkuu wa Mkoa

**Mkutano Mkuu wa Mkoa utakuwa na wajumbe wafuatao:-**

(a) Wajumbe wa Kamati ya Uendeshaji ya Mkoa
(b) Wajumbe wa Kamati za Utendaji za Wilaya
(c) Mwenyekiti wa Kitengo cha Walimu wanawake wa Mkoa
(d) Wajumbe wa vikao vya juu vya Chama walioko kwenye Mkoa husika isipokuwa Rais, Makamu wa Rais, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu Na Mweka Hazina WA Taifa

### 17.2 Baraza la Mkoa

Baraza la Mkoa litakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Wajumbe wa Kamati ya Uendeshaji ya Mkoa
(b) Wajumbe wa Kamati ya Uendeshaji ya kila Wilaya
(c) Mwenyekiti wa kitengo cha Walimu Wanawake wa Mkoa.

(d) Wajumbe wa vikao vya juu vya Chama walioko kwenye Mkoa husika isipokuwa Rais, Makamu wa Rais, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Mweka Hazina wa Taifa

### 17.3 Kamati ya Uendeshaji ya Mkoa

Kamati ya Uendeshaji ya Mkoa itakuwa na wajumbe wafuatao:

(a) Mwenyekiti wa Mkoa.
(b) Katibu wa Mkoa.
(c) Mweka Hazina wa Mkoa.
(d) Mwakilishi wa walimu wanawake wa mkoa.
(e) Mwakilishi wa walimu wenye ulemavu wa Mkoa.
(f) Mwakilishi wa walimu vijana wa Mkoa.

## 18. VIKAO VYA MKOA

### 18.1 Mkutano Mkuu wa Mkoa

(a) Mkutano Mkuu wa Mkoa utafanyika mara moja kila baada ya miaka mitano.
(b) Kikao cha dharura kinaweza kuitishwa ikibidi.

### 18.2 Baraza la Mkoa

(a) Baraza la Mkoa litakutana mara moja kila mwaka.

(b) Tarehe ya Mkutano itapangwa na Kamati ya Uendeshaji ya Mkoa.

### 18.3 Kamati ya Uendeshaji ya Mkoa

(a) Kamati ya Uendeshaji ya Mkoa itakutana mara moja kila baada ya miezi mitatu.

(b) Tarehe ya mkutano itapangwa na Katibu kwa kushirikiana na Mwenyekiti.

## 19. WAJIBU WA VIKAO VYA MKOA

### 19.1 Mkutano Mkuu wa Mkoa

Kazi za Mkutano Mkuu wa Mkoa zitakuwa kama ifuatavyo:

(a) Kupokea na kujadili taarifa ya kazi za Chama kwa kipindi cha miaka mitano kama itakavyowasilishwa na Baraza la Mkoa.

(b) Kupokea na kujadili taarifa ya mapato na matumizi ya fedha kwa kipindi cha miaka mitano kama itakavyowasilishwa na Baraza la Mkoa.

(c) Kuchagua viongozi na wawakilishi wa ngazi ya mkoa na Taifa kama ifuatavyo:-

i) Wajumbe wa Kamati ya Uendeshaji ya Mkoa
ii) Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Taifa
iii) Mwakilishi wa wenyeviti wa wilaya kwenye Baraza la Taifa

(d) Kupokea, kujadili na kuthibitisha mipango ya miaka mitano ya Chama ngazi ya Mkoa.

(e) Kuwaondoa madarakani viongozi uliowachagua wakipatikana na hatia baada ya kuwapa fursa ya kusikilizwa.

(f) Kuwachagua Wawakilishi wa Chama kwenye Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi kwa utaratibu utakaowekwa na Kanuni za Chama.

## 19.2 Baraza la Mkoa

(a) Kupokea, kujadili na kuthibitisha taarifa ya kazi za Chama kwakipindi cha mwaka mmoja kama itakavyowasilishwa na Kamati ya Uendeshaji ya Mkoa

(b) Kupokea,kujadili na kuthibitisha taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Chama kwa kipindi cha mwaka mmoja kama ilivyowasilishwa na Kamati ya Uendeshaji ya Mkoa.

(c) Kusimamia vyombo mali na Miradi ya kiuchumi ya ya Chama katika Mkoa

(d) Kuandaa mikakati ya utekelezaji wa mipango ya miaka mitano na kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Mkoa.

(e) Kujaza nafasi zilizowazi za uongozi katika Mkoa.

(f) Kuandaa Ajenda na tarehe ya Mkutano Mkuu wa Mkoa

(g) Kuwaondoa madarakani viongozi lililowachagua wakipatikana na hatia baada ya kuwapa fursa ya kusikilizwa.

### 19.3 Kamati ya Uendeshaji ya Mkoa.

(a) Kuendesha na kusimamia shughuli za Chama Mkoani.

(b) Kusimamia utekelezaji wa maazimio ya vikao vya juu.

(c) Kudhibiti na kuandaa taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Chama na kutoa taarifa kwa Baraza la Mkoa.

(d) Kushughulikia maendeleo ya walimu katika maslahi yao ya elimu na mafunzo, uimarishaji wa Chama, afya kazini, usafi wa mazingira na mengineyo katika kuinua hadhi ya taaluma ya Ualimu.

(e) Kuandaa mikakati ya utekelezaji wa mipango ya miaka mitatu.

(f) Kuratibu shughuli zote za Chama za Wilaya katika Mkoa.

(g) Kumsimamisha uongozi Kiongozi wa kuchaguliwa ngazi ya mkoa atakayekiuka taratibu za Chama au kufanya ubadhilifu wa mali na fedha za Chama katika ngazi ya mkoa na kupendekeza kwa Baraza la Mkoa hatua za kuchukua dhidi ya mhusika.

## 20.KAZI NA MADARAKA YA VIONGOZI WA MKOA

### 20.1Mwenyekiti

(a) Kiongozi Mkuu wa Chama katika Mkoa.

(b) Kuwa mwenyekiti wa vikao vyote vya Chama katika Mkoa na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya vikao vya Taifa.

(c) Kuwa Msemaji na mtetezi mkuu wa Chama katika Mkoa.

(d) Kutoa msimamo wa Sera za Chama kama zitakavyoamuliwa na vikao vya Chama kitaifa.

**20.2 Katibu**

(a) Kuitisha vikao vya Chama vya Mkoa kwa kushauriana na Mwenyekiti.

(b) Kusimamia shughuli zote za uendeshaji ikiwa ni pamoja na mapato na matumizi ya Chama.

(c) Kuwa Katibu wa vikao vyote na mikutano ya Mkoa.

(d) Kuweka kumbukumbu za shughuli za Chama katika Mkoa.

(e) Kufuatilia makato ya fedha za walimu kutoka kwa Makatibu wa wilaya zake.

(f) Kutunza mali za Chama.

(g) Kuandaa na kuwasilisha taarifa za shughuli za Chama katika kipindi husika.

(h) Mtendaji Mkuu wa Chama katika Mkoa.

(i) Kuhamasisha na kuingiza wanachama wapya.

**20.3. Mweka Hazina**

(a) Kuandaa na kutoa taarifa ya fedha za Chama katika vikao vya Mkoa kwa kushirikiana na Katibu.

(b) Kubuni mbinu za kuongeza mapato ya Chama katika ngazi ya Mkoa.

(c) Kuweka kumbukumbu sahihi ya mapato na matumizi ya Chama.

## 21 WAJUMBE WA NGAZI YA TAIFA

### 21.1 Mkutano Mkuu wa Taifa

Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Wajumbe wa Baraza la Taifa
(b) Wajumbe wa Kamati ya Uendeshaji ya kila Wilaya

**21.2. Baraza la Taifa**

Baraza la Taifa litakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(b) Kamati ya Uendeshaji ya kila Mkoa.

(c) Mwenyekiti wa Kitengo cha Walimu wanawake Taifa.

(d) Wadhamini wa Chama ambao watakuwa ni wajumbe wa kualikwa.

(e) Mwakilishi mmoja wa wenyeviti wa wilaya kutoka kila mkoa

**21.3. Kamati ya Utendaji ya Taifa**

Kamati ya Utendaji ya Taifa itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Rais

(b) Makamu Rais

(c) Katibu Mkuu

(d) Naibu Katibu Mkuu

(e) Mweka Hazina

(f) Mjumbe mmoja kutoka kila Mkoa

(g) Mwakilishi wa Walimu wenye ulemavu

(h) Mwakilishi wa Walimu wanawake

(i) Mwakilishi wa Walimu vijana

## 22. TARATIBU ZA VIKAO VYA TAIFA

**22.1. Mkutano Mkuu wa Taifa**

(a) Mkutano Mkuu wa Taifa utakuwa ndiyo Kikao Kikuu cha Chama chenye madaraka ya mwisho.

(b) Mkutano Mkuu wa Taifa wa kawaida utakuwepo mara mbili kila baada ya miaka miwili na nusu katika kipindi cha miaka mitano. Mkutano wa dharura utaitishwa umuhimu utakapojitokeza.

(c) Tarehe ya Mkutano itapangwa na Baraza la Taifa.

**22.2. Baraza la Taifa**

(a) Baraza la Taifa litakuwa na kikao chake mara moja kwa mwaka.

(b) Kikao cha dharura kinaweza kutishwa ikibidi

(c) Tarehe ya Baraza la Taifa itapangwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

**22.3. Kamati ya Utendaji ya Taifa**

(a) Kamati ya Utendaji ya Taifa itakuwa na vikao viwili (2) kwa mwaka.

(b) Kikao cha dharura kinaweza kutishwa ikibidi

(c) Tarehe ya kikao itapangwa na Katibu Mkuu kwa kushauriana na Rais.

## 23. WAJIBU WA VIKAO VYA TAIFA

**23.1. Mkutano Mkuu wa Taifa**

Kazi za Mkutano Mkuu wa Taifa zitakuwa kama ifuatavyo:-

(a) Kupokea,kujadili na kuthibitisha taarifa ya kazi za Chama kwa kipindi cha miaka miwili na nusu kama ilivyowasilishwa na Baraza la Taifa.

(b) Kupokea, kujadili na kuthibitisha taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Chama kwa kipindi cha miaka miwili na nusu kama itakavyowasilishwa na Baraza la Taifa.

(c) Kufanya mabadiliko ya Katiba kwa uamuzi wa theluthi mbili za wajumbe walio na haki ya kupiga kura.

(d) Kuwachagua viongozi wa Chama wafuatao:-

(i) Rais

(ii) Makamu wa Rais

(iii) Katibu Mkuu

(iv) Naibu Katibu Mkuu

(v) Mweka Hazina

(vi) Mwakilishi wa Walimu wenye ulemavu kwenye Kamati ya Utendaji ya Taifa

(vii) Mwakilishi wa Walimu vijana kwenye Kamati ya Utendaji ya Taifa

(viii) Mwakilishi wa Walimu wanawake kwenye Kamati ya Utendaji ya Taifa

(ix) Wadhamini watatu wa Chama

(e) Kupokea, kujadili na kupitisha mipango ya miaka mitano ya Chama.

(f) Kupitisha majina ya wanachama wa Heshima.

(g) Kupitisha Sera za Chama.

(h) Kuwaondoa madarakani viongozi uliowachagua wakipatikana na hatia baada ya kuwapa fursa ya kusikilizwa.

**23.2. Baraza la Taifa**

Baraza la Taifa litakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya kazi za Chama kwa kipindi cha mwaka mmoja kama ilivyowakilishwa na Kamati ya Utendaji.

(b) Kupokea, kujadili na kupitisha taarifa ya mapato na matumizi ya fedha za Chama kama ilivyowasilishwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(c) Kutoa mapendekezo kwa Mkutano Mkuu wa Taifa kuhusu mabadiliko yoyote katika katiba.

(d) Kupendekeza majina ya wanachama wa Heshima.

(e) Kutayarisha mipango ya miaka mitano ya Chama.

(f) Kutunga Kanuni mbalimbali za Chama kulingana na mahitaji na kuzirekebisha pindi inapobidi.

(g) Kujaza nafasi zilizo wazi za uongozi katika Taifa.

(h) Kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya viongozi wa kitaifa wanaochaguliwa na Mkutano Mkuu, hii ikiwa ni pamoja na kuonya na kuwasimamisha uongozi wakati ukisubiriwa uamuzi wa Mkutano Mkuu wa Taifa na kutoa mapendekezo kwa Mkutano Mkuu wa Taifa kwa kuamuzi wa mwisho.

(i) Kuteua Mkaguzi wa hesabu za fedha za Chama.

(j) Kuanzisha na kudhibiti mfuko wa dharura wa Taifa kwa kuzingatia Kanuni za fedha za Chama.

(k) Kuwasilisha kwenye Mkutano Mkuu wa Chama hesabu za fedha za Chama zilizokaguliwa.

**23.3. Kamati ya Utendaji ya Taifa**

Kamati ya Utendaji ya Taifa itakuwa na kazi zifuatazo:-

(a) Kuendesha na kusimamia shughuli za Chama.

(b) Kusimamia utekelezaji wa maazimio ya vikao vya juu.

(c) Kudhibiti mapato na matumizi ya fedha za Chama na kutoa taarifa kwa Baraza la Taifa.

(d) Kusimamia vyombo vya uchumi vya Chama.

(e) Kushughulikia maendeleo ya walimu katika elimu, mafunzo, uchumi, utafiti, mipango, fedha, utawala, sheria, uhusiano kazini, uimarishaji wa Chama, afya na usalama kazini, na mengineyo katika kuinua hadhi ya taaluma ya Mwalimu.

(f) Kuandaa agenda za mikutano ya Baraza la Taifa.

(g) Kamati ya Utendaji ya Taifa ina haki ya kufuta ujumbe wa mjumbe yeyote wa Kamati ya Utendaji au Kamati nyingine iwapo mjumbe atakosa kuhudhuria mikutano mitatu (3) mfululizo bila taarifa.

(h) Kupendekeza Mkaguzi Mkuu wa hesabu za fedha za Chama.

(i) Kuajiri watumishi wa Chama.

(j) Kuhakikisha kuwa hesabu za fedha za Chama zinakaguliwa kila mwaka na taarifa zinatolewa kwenye Baraza la Taifa.

**24. KAZI NA MADARAKA YA VIONGOZI WA TAIFA**

**24.1. Rais**

(a) Kiongozi Mkuu wa Chama.

(b) Kuwa Mwenyekiti wa vikao vyote vya Chama kitaifa na kufuatilia utekelezaji wa maamuzi ya vikao vya kitaifa.

(c) Kuwa Msemaji na mtetezi mkuu wa Chama.

(d) Kutoa msimamo wa Sera za Chama kama ilivyoamuliwa na vikao vya Chama vya Taifa.

**24.2. Makamu Rais**

(a) Naibu Kiongozi mkuu wa Chama.

(b) Kuongoza vikao vya Taifa kama Rais hayupo.

(c) Kuwa Msaidizi wa Rais wa Chama.

(d) Kuwa Kaimu wa Rais kama hayupo.

**24.3. Katibu Mkuu**

(a) Kuitisha vikao vya Kitaifa kwa kushauriana na Rais.

(b) Kusimamia shughuli za uendeshaji za kila siku za Chama.

(c) Kuwa Katibu wa vikao vyote vya Taifa.

(d) Kuweka kumbukumbu za shughuli zote za Chama.

(e) Kuhusika na utoaji wa vitambulisho kwa wanachama.

(f) Kufuatilia makato ya ada za wanachama kutoka kwa Makatibu wa Mikoa na Waajiri.

(g) Mkuu wa watumishi wote wa Chama.

(h) Kuandaa taarifa ya shughuli za Chama katika kipindi husika.

(i) Mdhibiti mkuu wa fedha na mali za Chama katika ngazi zote.

(j) Kupokea Kusimamia, kutunza na kugawa fedha zote za Chama katika ngazi husika kwa maelekezo yatakayotolewa na Baraza la Taifa.

**24.4. Naibu Katibu Mkuu**

(a) Naibu Katibu Mkuu atamsaidia Katibu Mkuu katika utekelezaji wa shughuli za Chama zilizoainishwa katika (c) ya kifungu hiki.

(b) Atakuwa Kaimu Katibu Mkuu wakati Katibu Mkuu hayupo.

**24.5. Mweka Hazina**

(a) Kusimamia mapato na matumizi ya fedha za Chama.

(b) Kuweka kumbukumbu sahihi ya mapato na matumizi ya Chama kwa kushirikiana na Katibu Mkuu.

(c) Kuandaa na kutoa taarifa ya mapato na matumizi ya Chama kwa Mkutano Mkuu wa Taifa, Baraza la Taifa na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(d) Kubuni mbinu za kuongeza mapato ya Chama.

(e) Kutunza mali za Chama kwa kushirikiana na Katibu Mkuu.

(f) Kuwa mweka sahihi katika hundi.

## 25. WADHAMINI WA CHAMA

**25.1. Wadhamini wa Chama watakuwa ni Walimu wenye heshima na nidhamu.**

(a) Mkutano Mkuu wa Taifa utachagua Wadhamini watatu kutokana na wanachama walio na umri wa miaka 35 na zaidi.

(b) Wadhamini watahudhuria vikao vya Baraza la Taifa kama Waalikwa.

(c) Wadhamini watachagua Mwenyekiti na Katibu kutoka miongoni mwao.

(d) Mali za Chama zitaandikishwa kwa jina la Baraza la Wadhamini.

(e) Mikataba yote, hati na dhamana za fedha za Chama zote zitamilikiwa kwa jina la Wadhamini na kuhifadhiwa na Katibu Mkuu.

(f) Wadhamini watalipwa posho ya kila mwezi kutokana na fedha za Chama, kwa viwango vitakavyoamuliwa na Baraza la Taifa.

(g) Kanuni za Chama zitafafanua majukumu ya Wadhamini wa Chama.

**25.2. Mwanachama ataacha kuwa mdhamini ikiwa:**

(a) Atafukuzwa Uanachama.

(b) Atakuwa hana akili timamu.

(c) Atavunja maadili

(d) Atajiuzulu.

(e) Atapatikana na kosa la jinai.

(f) Atastaafu.

(g) Atafariki.

(h) Atafikisha umri wa miaka 60

## 26. KITENGO CHA WALIMU WANAWAKE

(a) Kutakuwa na kitengo cha wanachama wanawake ambacho kitakuwa na Kamati za Jinsia na Walimu Wanawake katika ngazi ya Wilaya hadi ya Taifa. Kamati hizi zitafanya shughuli zake chini ya Katibu wa Chama wa ngazi husika kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

(b) Kabla ya vikao vya bajeti vya ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa, vitafanyika vikao vya Walimu Wanawake ambao ni wajumbe wa vikao hivyo.

(c) Viongozi wa Kamati za Jinsia na Walimu Wanawake katika ngazi mbalimbali watachaguliwa sambamba na uchaguzi wa viongozi wengine wa Chama.

(d) Kanuni za Chama zitafafanua utaratibu wa shughuli za Kitengo cha Walimu wenye ulemavu.

## 27. KITENGO CHA WALIMU WENYE ULEMAVU

(a) Kutakuwa na kitengo cha wanachama Walimu wenye ulemavu ambacho kitakuwa na Kamati zake katika ngazi ya Mkoa na ya Taifa. Kamati hizi zitafanya shughuli zake chini ya Katibu wa Chama

wa ngazi husika kwa mujibu wa Kanuni za Chama.

(b) Kabla ya vikao vya bajeti vya ngazi ya Wilaya, Mkoa na Taifa, vitafanyika vikao vya Walimu wenye ulemavu ambao ni wajumbe wa vikao hivyo.

(c) Viongozi wa Kamati za Walimu wenye ulemavu katika ngazi mbalimbali watachaguliwa sambamba na uchaguzi wa viongozi wengine wa Chama.

(d) Kanuni za Chama zitafafanua utaratibu wa shughuli za Kitengo cha Walimu wenye ulemavu.

## 28. TARATIBU ZA KUITISHA VIKAO

**28.1. Notisi ya Mikutano yote ya Chama itatolewa kwa maandishi na itaonesha:**

(a) Agenda za mkutano.
(b) Mahali pa kufanyia mkutano.
(c) Tarehe ya mkutano
(d) Siku ya mkutano.
(e) Saa ya mkutano.
(f) Maagizo mengine yatakayowahusu wajumbe watakaohudhuria mikutano hiyo.

## 29. UCHAGUZI NA MUDA WA UONGOZI

(a) Wakati wa uchaguzi ngazi zinazohusika zitachagua wajumbe wa Mikutano Mikuu, Mabaraza na Kamati za Utendaji, Kamati ya Uendeshaji, Kamati za Uratibu viongozi wa Tawi na wawakilishi sehemu za kazi.

(b) Muda wa uongozi kwa viongozi wa kuchaguliwa ndani ya Chama cha Walimu Tanzania (CWT) utakuwa ni miaka mitano.

(c) Kila nafasi ya uongozi inaweza kugombewa na mwanachama mwenye sifa kwa kipindi chochote.

## 30. WATUMISHI WA CHAMA

(a) Watumishi wa Chama watakuwa ni Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu pamoja na watumishi wengine watakaoajiriwa na Chama.

(b) Kamati ya Utendaji ya Taifa ndiyo Mamlaka ya ajira kwa watumishi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT).

(c) Watumishi wote watafanya kazi kwa mujibu wa mikataba yao ya ajira.

(d) Watumishi wa Chama watalipwa mishahara yao kutokana na fedha za Chama kwa viwango vitakavyopangwa na Kamati ya Utendaji ya Taifa.

(e) Watumishi wa Chama wa kuajiriwa hawatakuwa na haki ya kupiga kura isipokuwa watakuwa na haki ya kuchaguliwa kushika wadhifa wowote ndani ya Chama kwa utaratibu utakaowekwa na Kanuni za Chama.

## SEHEMU YA NNE

## FEDHA NA MALI ZA CHAMA

### 31. MAPATO YA CHAMA

#### 31.1. Ada za Uanachama

Ada ya Uanachama itakuwa ni kwa mujibu wa Katiba hii

#### 31.2. Michango

Kamati ya Utendaji ya Wilaya/Mabaraza ya Mikoa na Taifa yanaweza kuchangisha michango maalumu, kwa ajili ya miradi ya Chama baada ya kupata kibali kutoka kwa Baraza la Taifa au Kamati ya Utendaji ya Taifa.

#### 31.3. Mapato mengineyo

(a) Mauzo yatokanayo na mali ya Chama.

(b) Riba itokanayo na amana za Chama.

(c) Mapato yatokanayo na misaada ya Wahisani.

(d) Njia nyinginezo za mapato kama itakavyoamuliwa na kukubalika katika vikao.

(e) Ada ya huduma.

(f) Mapato yatokanayo na Miradi ya kiuchumi

### 32. MATUMIZI YA FEDHA ZA CHAMA

32.1. Fedha za Chama zitatumiwa kwa mambo yafuatayo:-

(a) Malipo ya mishahara, posho na gharama za maofisa wa Chama.

(b) Malipo ya mambo ya utawala wa Chama, ukaguzi wa fedha za Chama.

(c) Malipo ya kuendeshea kesi katika kulinda haki za Chama na mwanachama.

(d) Kutatua migogoro ya kikazi.

(e) Malipo ya adhabu yoyote iliyotolewa dhidi ya Chama.

(g) Malipo ya ushirikishwaji wa Chama.

(h) Uwekezaji kama itakavyoamuliwa na Baraza la Taifa.

(i) Malipo mengine halali kwa manufaa ya umma.

## 34. TARATIBU ZA UTUNZAJI WA FEDHA

34.1 Kamati ya Utendaji ya Taifa itawajibika kwa Baraza la Taifa katika uendeshaji na usimamizi wa fedha zote za Chama.

34.2 Katibu Mkuu/Katibu wa ngazi husika atafungua Akaunti katika Benki kwa jina la Chama na kuhakikisha kuwa fedha za Chama zote zinaingizwa katika Akaunti hizo.

34.3 Fedha zote za Chama zitakazopokelewa zitawekwa katika Akaunti ya Chama.

34.4 Katika utoaji wa fedha za Chama benki, wafuatao watahusika katika ngazi mbalimbali:

**(a) Wilaya**

(i) Katibu wa Wilaya
(ii) Mweka Hazina wa Wilaya
(iii) Wajumbe wawili watakaochaguliwa miongoni mwa viongozi wa Kamati ya Utendaji ya Wilaya isipokuwa Mwenyekiti wa Wilaya

**(b) Mkoa**

(i) Katibu wa Mkoa
(ii) Mweka Hazina wa Mkoa

(iii) Wajumbe wawili watakaochaguliwa miongoni mwa viongozi wa Kamati ya Uendeshaji Mkoa isipokuwa Mwenyekiti wa Mkoa.

**(c) Makao Makuu**

(i) Katibu Mkuu
(ii) Mweka Hazina wa Taifa
(iii) Mhasibu Mkuu
(iv) Kutakuwa na waweka saini mbadala ambao ni Naibu Katibu Mkuu na Mhasibu Mkuu Msaidizi.

(d) Saini za watu watatu ndizo zitakazotumika kutoa fedha benki ambao ni Katibu na Mweka Hazina wa ngazi husika na mmoja kati ya watia saini wengine wawili. Kanuni za Chama zitaweka utaratibu wa kutoa fedha katika sehemu za kazi na Vitengo mbalimbali vya Chama kwa kadri itakavyoonekana inafaa.

(e) Hesabu za fedha za Chama ni pamoja na fedha za Sehemu za Kazi, Vitengo, Wilaya, Mikoa na Taifa,

(f) Taratibu za utunzaji wa fedha zitahusisha ngazi zote zinazopokea fedha za Chama na zitafafanuliwa kwenye Kanuni za Fedha za Chama.

## 35. BAJETI YA MWAKA YA CHAMA

(a) Kamati ya Utendaji ya Wilaya itapitisha Bajeti ya Chama ngazi ya Wilaya.

(b) Baraza la Mkoa litapitisha Bajeti ya Mkoa

(c) Baraza la Taifa litapitisha Bajeti ya Chama ngazi ya Taifa.

(d) Mapato yatokanayo na Ada za Wanachama yatagawanywa kwa matumizi ya viwango maalumu kwa ngazi mbali mbali za Chama kama itakavyoamuliwa na Baraza la Taifa**.**

## 36. MALI ZA CHAMA

(a) Katibu Mkuu ataamua juu ya manunuzi, usambazaji na utunzaji wa mali za Chama kama itakavyoamuliwa na Baraza la Taifa.

(b) Mali zote za Chama zinazoondosheka na zisizoondosheka zitakuwa chini ya uangalizi na udhibiti wa Baraza la Wadhamini wa Chama.

## SEHEMU YA TANO

## MENGINEYO

### 37. KUPIGA KURA

(a) Kura zote zinazohusu uchaguzi zitafanywa kwa siri.

(b) Mwanachama kamili ndiye atakayehudhuria vikao anavyohusika na kuwa na haki ya kupiga kura.

(c) Watumishi wa Chama hawatakuwa na haki ya kupiga kura katika vikao vyote ambavyo wao ni wajumbe isipokuwa katika shughuli za Tawi la wafanyakazi na kwenye Baraza la wafanyakazi wa Chama.

### 38. UTATUZI WA MIGOGORO

Ikiwa kutakuwepo hali isiyokuwa ya maelewano kati ya mwajiri na mwanachama/mfanyakazi, wanachama kwa wanachama/wafanyakazi kwa wafanyakazi, ngazi ya uongozi inayohusika katika eneo la mgogoro itachukua hatua zinazostahili kwa kuzingatia taratibu za kutatua migogoro ambazo zimepitishwa na Baraza la Taifa kwenye Kanuni za Chama.

### 39. TAFSIRI YA KATIBA

Ikiwa matatizo yoyote yatatokea katika kutafsiri Katiba hii kutokana na kukosekana kwa kipengele au matatizo mengine, basi Kamati ya Utendaji ya Taifa itakuwa na uwezo wa kutafsiri Katiba hii kulingana na madhumuni yake. Tafsiri sahihi ya mwisho itatolewa na Baraza la Taifa kwa niaba ya Mkutano Mkuu wa Taifa.

### 40. MABADILIKO YA KATIBA

(a) Katiba hii inaweza kubadilishwa na Mkutano Mkuu wa Taifa baada ya theluthi mbili (2/3) ya

wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wenye haki ya kupiga kura kukubali mabadiliko hayo.

(b) Taarifa za mapendekezo au masahihisho ni lazima yawe yamemfikia Katibu Mkuu siku sitini (60) kabla ya kufunguliwa kwa Mkutano Mkuu ambao utajadili mapendekezo hayo. Kanuni za Chama zitaweka utaratibu wa kufuatwa kabla ya kuitishwa kwa Mkutano Mkuu wa Taifa kwa ajili ya marekebisho ya Katiba.

## 41. KANUNI ZA CHAMA

(a) Kutakuwa na Kanuni za Chama ambazo zitaenda sambamba na Katiba ya Chama. Pale ambapo patakuwa na utatanishi Katiba itatawala.

(b) Kanuni za Chama zitatungwa na Baraza la Taifa. Kanuni hizo zitaweka utaratibu wa kuitisha na kuendesha mikutano, kuweka Akidi na jinsi ya kutunza kumbukumbu za mikutano ya Chama.

## 42. MUDA WA KUKAIMU

Muda wa kukaimu nafasi ya uongozi katika Chama utakuwa si zaidi ya miezi kumi na miwili (12). Pale nafasi inapokuwa wazi kutokana na kufariki, kufukuzwa, kuhama au kujiuzulu, mamlaka husika zitabidi zijaze nafasi hizo kwa kutangaza nafasi wazi.

## 43. KUFUKUZWA UANACHAMA

### 43.1 Sababu za kufukuzwa uanachama

Mwanachama ikiwa ni pamoja na Kiongozi wa kuteuliwa, atafukuzwa Uanachama kama:-

(a) Amejipatia Uanachama kwa hila, ujanja au kudanganya.
(b) Amethibitika kutumia fedha za Chama kwa ubadhilifu, na kupoteza au kuharibu mali ya Chama. Inapobidi atachukuliwa hatua za kisheria.
(c) Ni mwanachama wa Chama kingine cha Wafanyakazi.

(d) Ametenda vitendo vinavyopingana na Katiba au maamuzi ya Mkutano Mkuu wa Taifa.

(e) Amethibitika kuwa msaliti wa Chama.

**43.2 Utaratibu wa kufuatwa kabla ya kufukuzwa uanachama Kama itabidi kumfukuza mwanachama Uanachama, utaratibu ufuatao utatumika:-**

(a) Mapendekezo yatatoka kwenye Kamati ya Utendaji ya Wilaya, Baraza la Mkoa na yatawasilishwa kwenye Baraza la Taifa kwa uamuzi.

(b) Katibu Mkuu atawasiliana na mwanachama kwa maandishi kuhusu uamuzi.

## 44. KUJAZA NAFASI ZILIZO WAZI ZA UONGOZI

(a) Nafasi ya uongozi itahesabiwa kuwa iko wazi endapo kiongozi anayehusika atakuwa:

(i) Amekosa sifa za kuwa kiongozi.

(ii) Amejiuzulu.

(iii) Hana akili timamu.

(iv) Amefukuzwa uongozi.

(v) Amestaafu

(vi) Kufariki

(vii) Ametimiza umri wa miaka sitini (60)

44.2 Utaratibu wa kujaza nafasi zilizowazi utafafanuliwa kwenye Kanuni za Chama.

## 45. TAWI NA BARAZA LA WAFANYAKAZI

(a) Kutakuwa na tawi maalumu la wafanyakazi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT).

(b) Kutakuwa na Baraza la Wafanyakazi wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), litakalokuwa na jukumu la kumshauri Mwajiri kuhusu namna ya kuboresha maslahi ya watumishi na kuongeza tija.

## 46. KUFUTA CHAMA CHA WALIMU TANZANIA (CWT)

(a) Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kinaweza kufutwa au kufungiwa kuendesha shughuli zake baada ya uamuzi huo kukubaliwa na theluthi mbili (2/3) ya wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa wenye haki ya kupiga kura.

(b) Maamuzi ya kufuta Chama cha Walimu Tanzania (CWT) ni lazima yaelezee mgawanyo wa mali za Chama kama Baraza la Taifa na Wadhamini wa Chama watakavyopendekeza kwa kuzingatia sheria za nchi.

## 47. MGOMO

Ni haki ya Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kuitisha mgomo pale inapobidi. Kabla ya kuitisha mgomo, wanachama watatakiwa kupiga kura kuamua mgomo uitishwe au la na kuridhiwa na Baraza la Taifa baada ya kupokea mapendekezo kutoka kwenye Kamati ya Utendaji ya Taifa. Kanuni za Chama zitatoa utaratibu wa kuendesha kura ya kuamua juu ya mgomo.

## 48. KUUNGANA NA AU KUUNDA SHIRIKISHO

(a) Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kinaweza kuungana na Chama au vyama vingine na au kujishirikisha na Shirikisho lolote ndani na nje ya nchi.

(b) Endapo Chama kitajishirikisha na Shirikisho lolote ndani na au nje ya nchi, wajumbe wa mikutano ya Shirikisho husika watachaguliwa miongoni wa wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa.